**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**MANISPAA YA SINGIDA**

**MTIHANI WA AWALI KABLA YA MTIHANI WA TAIFA**

KIDATO CHA NNE

KISWAHILI

Muda:3:00 Agosti,2023.

.......................................................................................................................................

MAELEKEZO

- Mtihani huu una sehemu A,B na C zenye jumla ya maswali 11
- Jibu maswali yote kutoka sehemu A na B na maswali mawili(02)kutoka sehemu C
- Swali la 10 ni la lazima
- Mpango mzuri wa kazi,mwandiko safi vinashawishi kwenye alama
- Andika namba yako ya mitihani kwenye kila kurasa ya karatasi yako ya kujibia
- Zingatia maagizo ya kila sehemu na kila swali
- Vifaa vyote vya mawasiliano na vitu visivyoruhusiwa havitakiwi katika chumba cha mitihani

| NAMBA YA SWALI | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 | 6 | 7 | 8 | 9 | 10 | 11 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| WEKA (√) | | | | | | | | | | | |

Sehemu A(Alama 16)
Jibu maswali yote

1.Chagua herufi ya jibu sahihi katika sehemu uliyopewa

(i) Obogo alifurahi alipopata maswali yote ya Kiswahili.Neno lililopigiwa mstari ni

(a) Nomino (b) Kielezi (c) Kitenzi (d) Mofimu (e) Kishazi ( )

(ii)”Juma ameoa”,”Yahaya ameoa?”na “shabani kaoa!” katika utoaji wa sauti kipi ni sahihi ukizingatia hizo tungo tatu hapo juu?

(a)Mkazo (b)Lafudhi (c)Kiimbo (d)Matamshi (e)Alama za uandishi ( )

(iii)Utoaji wa misimu katika jamii hutegemea na;

(a)Uchaguzi wa viongozi (b)Mabadiliko ya jamii (c)Shughuli itendekayo

(d)Utani uliopo miongoni mwa wanajamii (e)Kutumika na kudumu kwa muda mrefu ( )

(iv) Mende anapenda kula uchafu.Neno uchafu lililopigiwa mstari lipo katika ngeli ipi?

(a) KI-VI (b) U-I (c) YU-A-WA (d) KU (e)LI-YA ( )

(v)Hamisi ni mwimbaji wa mashairi kila akiimba mashairi yake mshororo wa mwisho katika beti zake haubadiliki katika beti zote anapoimba,mshororo huo usiobadilika tunaweza kuupa jina gani kati ya haya kishairi?

(a)Mshororo takriri (b)Mshororo uradidi (c)Bahari (d)Kituo bahari (e)Kituo ( )

(vi)Utenzi:

(a)Utungo wa kishairi unaoeleza kwa urefu kuhusu wimbo

(b)Utungo wa kishairi unaoeleza kwa urefu kuhusu shairi

(c)Utungo wa kishairi mrefu unaoeleza kwa urefu kuhusu Ngonjera

(d)utungo wa kishairi unaoeleza kwa urefu kuhusu majigambo

(e)Utungo wa kishairi unaoeleza kwa urefu kuhusu matukio ya kihistoria ( )

(vii)Ipi kati ya zifuatazo **SI** sifa ya ngonjera

(a)Huwa na vina ,mizani na urari (b)Huwa na mhusika mmoja (c)Huwa na malumbano
(d) Hutamkwa mbele ya hadhira (e)Hupatikani katika maigizo na mashairi ( )

(viii)Chagizo katika uchambnuzi wa sentensi hutumika katika mkabala wa:

(a)Kimuundo (b)Kimapokeo (c)Kisiasa (d)Kiupatanishi (e)Kisintaksia ( )

(ix)Neno cheza ni kitenzi kikuu na kitenzi kikuu huunda kishazi huru, na kishazi tegemezi vilevile ,huundwa na kitenzi ila utofautiwake ni kwamba

(a)Kishazi tegemezi huundwa na vitenzi vyenye viambishi vya o-rejeshi

(b)Kishazi tegemezi huundwa na vitenzi vyenye viambishi vilivyorejeshwa

(c)Kishazi tegemezi huundwa na sehemu ya kiarifu inayokaliwa na kielezi

(d)Kishazi tegemezi ni sehemu ya kiarifu inayokaliwa na Nomino

(e)Kishazi tegemezi ni mada ya sarufi tegemezi ( )

(x)Lahaja ya kishela inazungumzwa katika eneo lipi kati ya haya

(a)Tanga (b)Mombasa (c)Unguja mjini (d)Kisiwa cha pemba (e)Kisiwa cha lamu ( )

2.Oanisha kifungu cha maneno kutoka orodha A na maneno kutoka orodha B

| ORODHA A | ORODHA B |
|---|---|
| i. Lugha ya kibantu<br>ii. Katambuga,kifaru na nyau | A. Kumbukumbu za mkutano<br>B. Akronimia |

| | |
|---|---|
| iii. Uambatanishaji<br>iv. Gazeti la utawala wa kingereza<br>v. Muhtasari wa mambo muhimu yanayojadiliwa na kukubaliana katika mkutano.<br>vi. Humtofautisha na wasanii wengine wa jamii yake | C. Habari leo<br>D. Habari za leo<br>E. ufananisho<br>F. Njugumawe<br>G. Kiswahili<br>H. Mtindo<br>I. Muundo |

SEHEMU B(Alama 54)

Jibu maswali yote katika sehemu hii

3. Ashura ameingia kidato cha tatu mwaka huu,mwalimu kawapa kazi ya nyumbani watumie njia ngoe kwa kuzingatia mkabala wa kikazi wachanganue maneno haya aliyomwambia mwalimu hashimu kwenye simu"Wanafunzi wa kidato cha kwanza wanacheza mpira wakati wanafunzi wengine wanaimba nyimbo"wewe kama mwanafunzi wa kidato cha nne msaidie Ashura kukamilisha kazi aliyopewa na mwalimu

4.Kitanda mahali pake chumbani,sufuria mahari pake jikoni,panga Nomino zifuatazo katika makundi ya Ngeli zake kwa kigezo cha kisintaksia

i. Kisu
ii. Chupa
iii. Mtoto
iv. Uovu
v. Mkutano
vi. Kusoma
vii. Mkasi
viii. Simu
ix. Samaki

5.Chunguza vifungu vya maneno vifuatavyo kisha fikiria methali ya utumizi itakayoweza kusimama na kutumika kama sehemu ya katazo au onyo katika utaratibu wa maisha wa kila siku. Tumia methali hiyo kurudia utenzi wa sentensi husika

i. Kama umekwama usilazimishe omba ushauri kwa wazee au viongozi wanaweza kukupa mwongozo
ii. Ni lazima muonyeshe ushirikiano katika hili kila mtu akifanya peke yake mambo yatakuwa magumu hamtafanikiwa
iii. Usifanye jambo hili kwa haraka,nenda polepole ili ufanye kwa ufanisi
iv. Acha kutumia pesa vibaya ukimaliza zote leo kesho nani atakupa,kwanini usihifadhi kidogo au unaona amna umuhimu
v. Mwenzio amesharidhika hawezi jua shida zako,Mngekuwa mnaangaika pamoja naye asingeziisi shida zako,kwaiyo pambana na hali yako
vi. Wengi wanasema ni mdokozi ingawa hatujawahi kumshuhudia akifanya hivyo, yeye mwenyewe ukimuuliza anakataa

6.”Lucas alimwambia mwanae kuwa katika ulimwengu huu,kila kitu kina chimbuko na asili yake.Kiswahili nacho kina asili yake kinadharia”.Kwa mifano madhubuti,thibitisha kauli hii kwa kutoa hoja nne.

7.Vyombo vya habari huwa na mchango  mkubwa katika kukuza lugha ya Kiswahili.Kwa mifano halisi,thibitisha dai hili kwa kutaja na kueleza kwa ufupi vyombo vya habari vinne,namna vinavyosaidia kukuza lugha ya Kiswahili.

8.Lahaja zifuatazo ni za pwani ya Afrika mashariki,kitikuu,kisiu.kipate,kiamu,kijomvu na kingare,kivumba,kipemba na kiunguja.Unafikiri ni kwa vipi lahaja hizi zinaweza kuchangia kustawi kwa Kiswahili.Toa hoja nne(4).

SEHEMU(Alama 30)

Jibu maswali mawili tu

9.Mzee Juma alimsimulia hadithi mjukuu wake kuhusu Fisi mla watu wa kijiji cha bweri. Mzee Musa alinunua kitabu chenye hadithi hiyohiyo akampa mjukuu wake John akisome.Tofautisha hadhira ya Mzee Juma na hadhira ya Mzee Musa,kwa kutoa hoja nne(4).

10.Chagua mashairi matatu kwa kila Diwani kutoka katika diwani mbili ulizosoma kisha onyesha jinsi washairi walivyo walimu bora kwa jamii ya leo.

11.Kwa kutumia riwaya mbili ulizosoma,fafanua jinsi waandishi wa riwaya,wanavyoibua na kuweka wazi mambo mbalimbali yanayoikabili jamii,ambayo yanakwamisha ujenzi wa jamii mpya.Toa hoja tatu kwa kila kitabu.